**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA MAKAMU WA RAIS**

# TAARIFA YA MKATABA WA USIMAMIZI ENDELEVU WA ZIWA TANGANYIKA (THE CONVENTION ON SUSTAINABLE MANAGEMENT OF LAKE TANGANYIKA)

**JANUARI, 2026**

## 1. UTANGULIZI

Mkataba wa Ziwa Tanganyika ni makubaliano ya kikanda yaliyoanzishwa tarehe 12 Juni, 2003 kwa lengo la kuimarisha usimamizi endelevu wa hifadhi ya mazingira ya Ziwa Tanganyika na Bonde lake. Mkataba huu unahusisha nchi nne zinazopakana na Ziwa Tanganyika ambazo ni Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (asilimia 45), Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (asilimia 41), Jamhuri ya Burundi (asilimia 8) na Jamhuri ya Zambia (asilimia 6). Tanzania iliridhia rasmi mkataba huu mwaka 2004, ikiwa ni ishara ya dhamira yake katika kulinda na kusimamia rasilimali za Ziwa Tanganyika kwa manufaa ya sasa na ya vizazi vijavyo.

## 2. Lengo la mkataba

Lengo kuu la Mkataba wa Ziwa Tanganyika ni kuhakikisha uhifadhi na matumizi endelevu ya maliasili za ziwa na mazingira yanayolizunguka kupitia misingi ya usimamizi jumuishi na ushirikiano wa kikanda. Aidha, mkataba unalenga kulinda bayoanuwai ya ziwa, kuzuia uharibifu wa mazingira, na kuhakikisha kuwa jamii zinazoishi karibu na Ziwa Tanganyika zinanufaika moja kwa moja na matumizi endelevu ya rasilimali na huduma za ziwa hilo.

## 3. Itifaki zilizo chini ya Mkataba wa Ziwa Tanganyika

Ili kufanikisha utekelezaji wa Mkataba wa Ziwa Tanganyika wa mwaka 2003, nchi wanachama zilikubaliana kuandaa na kutekeleza itifaki mbalimbali zinazolenga kusimamia maeneo mahsusi ya uhifadhi na matumizi endelevu ya rasilimali za ziwa. Itifaki hizi zinaweka miongozo ya kisheria na kiutawala kwa ajili ya kulinda mazingira ya Ziwa Tanganyika na kuhakikisha manufaa ya pamoja kwa nchi wanachama na jamii zinazolizunguka ziwa. Itifaki kuu zilizo chini ya Mkataba huu ni kama ifuatavyo:

3.1 Itifaki ya Usimamizi Endelevu wa Uvuvi wa Ziwa Tanganyika

Itifaki hii inalenga kuhakikisha kuwa shughuli za uvuvi katika Ziwa Tanganyika zinafanyika kwa njia endelevu ili kulinda hifadhi ya samaki na bayoanuwai ya majini. Inatambua kuwa uvuvi ni chanzo muhimu cha chakula, ajira na kipato kwa jamii zinazozunguka ziwa, hivyo inasisitiza uwiano kati ya matumizi na uhifadhi wa rasilimali za uvuvi.

Itifaki hii inaelekeza nchi wanachama kushirikiana katika:

- Kudhibiti uvuvi haramu, usioripotiwa na usiodhibitiwa;
- Kuweka na kusimamia kanuni za uvuvi kama vile ukubwa wa nyavu, aina za zana za uvuvi na misimu ya uvuvi;
- Kufanya tafiti za kisayansi kuhusu hifadhi ya samaki;
- Kujenga uwezo wa wavuvi na taasisi zinazohusika na sekta ya uvuvi.

3.2 Itifaki ya Udhibiti wa Uchafuzi wa Mazingira ya Ziwa Tanganyika

Itifaki hii inalenga kuzuia, kudhibiti na kupunguza uchafuzi wa mazingira ya Ziwa Tanganyika unaotokana na shughuli za binadamu kama vile kilimo, viwanda, makazi ya watu, usafirishaji majini na uchimbaji wa madini. Uchafuzi huu unatishia afya ya viumbe wa majini, ubora wa maji na maisha ya binadamu wanaotegemea ziwa.
Kupitia itifaki hii, nchi wanachama zinawajibika:

- Kuweka sera na sheria za kudhibiti utiririshaji wa taka na kemikali hatarishi kuingia ziwani;
- Kusimamia matumizi ya mbolea na viuatilifu katika maeneo ya bonde la ziwa;
- Kuimarisha mifumo ya usimamizi wa taka na maji taka;
- Kubadilishana taarifa na teknolojia bora za udhibiti wa uchafuzi.

3.3 Itifaki ya Uhifadhi wa Bayoanuwai na Usimamizi wa Maliasili za Ziwa Tanganyika

Itifaki hii inalenga kulinda na kuhifadhi bayoanuwai ya kipekee ya Ziwa Tanganyika, ambalo linajulikana kuwa miongoni mwa maziwa yenye viumbe wengi wa aina adimu duniani. Itifaki inasisitiza umuhimu wa kulinda makazi ya viumbe wa majini na nchi kavu yanayohusiana na ziwa.
Kupitia itifaki hii, nchi wanachama zinahimizwa:

- Kutambua na kulinda maeneo muhimu ya ikolojia;
- Kudhibiti shughuli za kibinadamu zinazohatarisha makazi ya viumbe hai;
- Kuhifadhi spishi zilizo hatarini kutoweka;
- Kushirikisha jamii katika shughuli za uhifadhi na matumizi endelevu ya maliasili.

3.4 Itifaki ya Ushirikiano wa Kikanda katika Utekelezaji na Ufuatiliaji

Itifaki hii inalenga kuimarisha ushirikiano wa kikanda kati ya nchi wanachama katika utekelezaji wa Mkataba wa Ziwa Tanganyika. Inahimiza ubadilishanaji wa taarifa, uzoefu na teknolojia, pamoja na uratibu wa sera na mipango ya usimamizi wa ziwa.

## 4. Uratibu wa Shughuli za Mkataba

Uratibu wa utekelezaji wa Mkataba wa Ziwa Tanganyika nchini Tanzania unafanywa na Ofisi ya Makamu wa Rais (OMR), ambayo hutumika kama Ofisi Kiungo kati ya Sekretarieti ya Mkataba wa Ziwa Tanganyika na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kupitia jukumu hili, OMR inahakikisha kuwa malengo, mikakati na majukumu yaliyoainishwa katika Mkataba na itifaki zake yanatekelezwa ipasavyo katika ngazi za kitaifa, kikanda na kijamii.

Kwa muktadha huo, OMR inawajibika kuratibu na kusimamia utekelezaji wa shughuli zote zinazohusiana na Mkataba wa Ziwa Tanganyika nchini, kwa kushirikiana na wizara, taasisi za umma, mamlaka za serikali za mitaa, sekta binafsi na wadau wengine muhimu. Uratibu huu unalenga kuhakikisha mshikamano wa kisera, matumizi bora ya rasilimali na ushiriki mpana wa wadau katika kulinda na kusimamia mazingira ya Ziwa Tanganyika kwa njia endelevu.

## 5. Majukumu ya Nchi Wanachama chini ya Mkataba wa Ziwa Tanganyika

Chini ya Mkataba wa Ziwa Tanganyika, nchi wanachama zinawajibika kutekeleza majukumu mbalimbali ya kifedha, kiutawala, kiufundi na kisera kwa lengo la kuhakikisha usimamizi endelevu wa rasilimali za ziwa kwa manufaa ya pamoja. Majukumu haya yanasisitiza mshikamano wa kikanda, uwajibikaji wa pamoja na utekelezaji wa maamuzi yanayofikiwa kwa makubaliano ya nchi wanachama.

## 6. Ushiriki wa nchi katika Mikutano

Nchi wanachama zina jukumu la kushiriki kikamilifu katika mikutano ya kikanda iliyo chini ya Mkataba, ikiwemo Mikutano ya Mawaziri wa Mkataba wa Ziwa Tanganyika inayofanyika kila mwaka. Mikutano hii ni jukwaa muhimu la kujadili hali ya mazingira ya ziwa, maendeleo ya utekelezaji wa mkataba, changamoto zinazojitokeza na mikakati ya pamoja ya kukabiliana nazo. Ushiriki wa nchi wanachama katika mikutano hii huchangia katika kufanya maamuzi ya pamoja, kuimarisha ushirikiano wa kikanda na kuhakikisha maslahi ya kila nchi yanazingatiwa katika usimamizi wa ziwa.

Ushiriki katiaka vikao vya maamuzi. Nchi wanachama zina wajibu wa kushiriki katika vikao vyote vya maamuzi vinavyoandaliwa chini ya Mkataba wa Ziwa Tanganyika, ikiwemo Mikutano ya Mawaziri na vikao vya kitaalamu. Ushiriki huu unahakikisha kuwa nchi zinachangia kikamilifu katika kupanga mwelekeo wa utekelezaji wa mkataba na kutoa maoni kuhusu sera, mikakati na programu za kikanda.

## 7. Vyombo vya Utekelezaji wa Mkataba wa Ziwa Tanganyika

9.1 Mkutano wa Mawaziri wa Mkataba wa Ziwa Tanganyika (CoM–LTA)
Mkutano wa Mawaziri wa Mkataba wa Ziwa Tanganyika ndio chombo cha juu kabisa cha maamuzi chini ya Mkataba. Kazi yake kuu ni kutathmini utekelezaji wa shughuli zote za Mkataba wa Ziwa Tanganyika, kutoa mwelekeo wa kisera na kupitisha maazimio muhimu yanayohusu usimamizi endelevu wa ziwa. Mkutano huu hufanyika mara moja kila mwaka na huhusisha mawaziri kutoka nchi wanachama wa Mkataba.

9.2 Kamati ya Usimamizi wa Mkataba wa Ziwa Tanganyika (MC–LTA)
Kamati ya Usimamizi wa Mkataba inaundwa na wajumbe wanne (4) kutoka kila nchi mwanachama. Kamati hii ina jukumu la kuratibu, kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa Mkataba kwa kuzingatia maelekezo na maazimio ya Mkutano wa Mawaziri. Mikutano ya Kamati ya Usimamizi hufanyika mara mbili (2) kwa mwaka. Ikumbukwe kuwa mikutano hii hutanguliwa na mikutano ya Watalaamu (Technical Committee), ambayo huchambua masuala ya kiufundi na kutoa mapendekezo kwa Kamati ya Usimamizi.

9.3 Sekretarieti ya Mkataba wa Ziwa Tanganyika (LTAS)
Sekretarieti ya Mkataba wa Ziwa Tanganyika ni chombo cha kiutendaji cha Mkataba. Ina jukumu la kuratibu utekelezaji wa shughuli zote za Mkataba, ikiwemo utekelezaji wa Mpango Mkakati wa Utekelezaji (Strategic Action Programme – SAP). Aidha, Sekretarieti ina wajibu wa kuandaa mipango ya kazi na bajeti, kuandaa na kuratibu utekelezaji wa miradi, pamoja na kufanya tathmini na kuandaa ripoti za utekelezaji kwa ajili ya vyombo vya maamuzi.

**8. Faida za utekelezaji wa shughuli za mkataba wa tanganyika**

i. Nchi kuweza kusimamia na Kudhibiti shughuli za uvuvi haramu katika ya Ziwa Tanganyika kupitia doria za mara kwa mara

ii. Tanzania kupata fedha kwa ajili ya kuimarisha uhifadhi wa Bioanuai katika Ziwa Tanganyika ambapo kupitia mradi wa LATAFIMA mwaka 2024 nchi ilipata Boti (2) za kufanyia doria.

iii. Kuimarika kwa ushirikiano miongoni mwa nchi wanachama katika kufanya utafiti na uendelezaji wa teknolojia za kusimamia na kuhifadhi Ziwa Tanganyika;

iv. Kuhakikisha msimamo na maslahi ya nchi yanawasilishwa kwenye mkutano na yanajumuishwa katika maazimio ya mkutano na mipango ya Mkataba huu;

v. Kukubalika kuwepo kwa nafasi ya Makatibu Wakuu katika muundo wa Mamlaka ya Usimamizi wa Ziwa Tanganyika ambapo awali nafasi hiyo haikuwepo;

vi. Kuwezesha lugha ya kiswahili kuwa miongoni mwa lugha tatu (3) ya mawasiliano katika mikutano ya nchi wanachama, hii ni agenda ya Tanzania.

vii. Jamii inayozunguka Ziwa kujengewa uelewa kuhusu hifadhi ya Ziwa Tanganyika

**9. Fursa zilizopo**

a) Tanzania kupata fursa ya kuteua mtaalamu atakaechukua nafasi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Sekretarieti kuanzia mwaka 2026 ambayo inafasi kubwa ya kiutendaji katika Mkataba

b) Tanzania kupata fedha za kigeni kwakuwa Mwenyeji wa Mikutano chini ya Mkataba

c) Kupata fursa ya Uvuvi endelevu ambayo itatokana na uridhiwaji wa Itifaki ya Ufugaji wa Samaki (Lake Taganyika Protocol on Aquaculture).

d) Uwepo wa Mradi wa Kuhifadhi Bioanuai, Matumizi Endelevu ya Ardhi na Usalama wa Maji (Biodiversity Conservation, Sustainable Land Management and Enhanced Water Security in Lake Tanganyika basin). Mradi huu ni wa kikanda na unathamani ya Dola za Kimarekani 14,590,000 kwa ufadhili wa Mfuko wa Mazingira wa Dunia (GEF). Kwa upande wa Tanzania, mradi utagharimu USD 3,604,934

    i. Mradi unatekelezwa na Ofisi ya Huduma za Miradi ya Umoja wa Mataifa (UNOPS)

    ii. Kipindi cha Utekelezaji 2024-2028

    iii. Unatekelezwa katika Mkoa wa Kigoma ( Wilaya ya Kibondo, Uvinza na Kasulu)

    iv. Mradi huu upo katika hatua za awali (inception phase) ambapo utaanza rasmi mwezi Septemba, 2025

    v. Shughuli zilizofanyika mpaka sasa ni pamoja na kuwatambua wadau wa mradi, NRG kwa ajili ya hatua zingine

## 10. Changamoto

Utekelezaji wa mkataba huu unakabiliwa na changamoto kadhaa, hasa katika kushughulikia masuala ya Usimamizi na uendelezaji wa mazingira na Uvuvi haramu kama ifuatavyo;

i. Ongezeko la uchafuzi wa mazingira ya Ziwa Tanganyika unaotokana na shughuli mbalimbali; ikiwemo taka zisizotibiwa, mtiririko wa mabaki yatokanayo na kilimo, uchafuzi uanotokana na taka za plastiki na uchafuzi wa taka za viwandani zinazoelekezwa baharini.
ii. Ukosefu wa takwimu na ufuatiliaji hali ambayo huzuia usimamizi bora wa mifumo ya ikolojia wa Ziwa.
iii. Mabadiliko ya taabianchi, ambapo vyanzo mbalimbali vimekuwa vikibainisha kuongezeka kwa mmomonyoko ardhi kwa kiwango kikubwa unaotishia mifumo ikolojia.

## HITIMISHO

(OMR) itaendelea kusimamia Mkataba huu kwa ufanisi ili kuimarisha ushirikiano wa kikanda katika kuratibu uhifadhi wa Mazingira ya Ziwa Tanganyika na kuwezesha nchi kunufaika na rasilimali ya Ziwa katika eneo husika na kupata fedha za kutekeleza miradi mbalimbali ya usimamizi na uendelezaji wa mazingira ya Ziwa. Aidha, kuwezesha nchi kunufaika na fursa za kujenga uwezo kitaasisi na kitaalamu katika kusimamia, kuhifadhi na kuendeleza mazingira ya Ziwa Tanganyika.